

DHANA YA UHUSIKA KATIKA KAULI YA KUTENDEA

Deo Ngonyani

Ikisiri

Dhana ya uhusika ina utata katika machapisho wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu wakati mwingine ikifasiliwa kuwa ni dhana ya kimuundo, na wakati mwingine, ni dhana ya kisemantiki. Makala hii inapendekeza kuichukulia dhana hiyo kuwa ni ya kimuundo na dhana ya ushiriki kuwa ni ya kisemantiki. Dhana hizo mbili zinaelezwa kwa kutumia mifano kutoka kauli ya kutendea. Unyambulishaji wa kutendea husababisha kitenzi kupata yambwa mpya. Yambwa mpya inaweza kutafsiriwa kwa namna mbalimbali kutokana na uhusiano wa yambwa hiyo na kitenzi. Kwa kutumia uhusiano mbalimbali wa yambwa na vitenzi, inaonesha kwamba uhusika wa ala waweza kuwa wa namna mbalimbali. Ushahidi unaotokana na uchambuzi wa sentensi za utendea na yambwa mbadala unadhihirisha kwamba tofauti za ushiriki zinatokana na maana ya mzizi wa kitenzi na hulka za nomino ninazohusika katika matukio.

Utangulizi

Dhana ya uhusika imekuwa na utata miongoni mwa wanaisimu. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* inasema uhusika ni dhana ya kisarufi itumikayo kuonyesha dhima ya maneno katika tungo (TUKI, 1990). Fasili hii inaashiria kwamba uhusika ni dhana inayoelezea uhusiano wa kimuundo. Katika *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, inaelezwa kwamba uhusika ni kategoria ya kisarufi itumikayo katika uchanganuzi wa sentensi kuonyesha uhusiano wa maneno yaliyomo katika tungo hiyo (Massamba 2004:97). Kwa hivyo, mwandishi anatoa mifano ya uhusika huo kama:

- (1) Uhusika (Massamba, 2004)
 - a. Uhusika kiima (*nominative case*)
 - b. Uhusika jumui (*ablative case*)
 - c. Uhusika mtendi (*agent case*)
 - d. Uhusika tendea (*dative case*)
 - e. Uhusika yambwa (*accusative case*)
 - f. Uhusika ala (*instrumental case*)

Tayari utata unaonekana hapa, kwani wakati “kiima” ni dhana ya kimuundo, “mtendi” inaelekea zaidi kuwa ni dhana ya kisemantiki. Khamis (2008) anataja aina kadha za uhusika, zikiwemo:

- (2) Dhima za kisemantiki
 - a. utenda

- b. utendeka
- c. ala
- d. hisi
- e. mahala
- f. lengo
- g. muawana
- h. tuko
- i. utendwa
- j. kisa
- k. jalizo

Orodha kama hii imo katika sura ambayo Habwe na Karanja (2004) wanaiita Semantiki. Matinde (2012) naye anasema uhusika ni kategoria ya kisarufi ambayo huonesha uhusiano wa viambajengo katika tungo. Aidha, huonesha uamilifu wa kila kiambajengo katika tungo na athari ya kiambajengo hicho na viambajengo vingine. Anaorodhesha uhusika huo kama uhusika kiima, uhusika tendea, uhusika ala, uhusika yambwa, uhusika mahali na uhusika mtenda au mtendewa. Mifano inayotolewa baada ya tafsiri inadhihirisha utata zaidi.

- (3) a. Mtoto mkorofi alipigwa na polisi. (uk. 208)
- b. Yeye alifukuzwa na mwalimu mkuu. (uk. 208)
- c. Mtoto alipigwa na mama yake. (uk. 209)

Kiima katika (3a) kinafafanuliwa kuwa na uhusika kiima. Lakini kiima katika (3b) kinaelezwa kuwa uhusika tendea, na kile cha (3c) kinatajwa kuwa ni uhusika mtendwa. Kwa hakika, virai vyote vitatu ni viima katika sentensi hizo. Hii ni kwa mujibu wa nafasi ya kiuamilifu. Virai hivi vinaonesha upatanisho wa kiima kwenye kitenzi. Utendea na utendwa ni uhusika wa kisemantiki. Utata huu ndiyo mada ya makala hii.

Lengo la makala hii ni kufufua mjadala kuhusu dhana hii kwa matumaini kwamba, hatimaye, tuatue utata huu. Ninapendekeza kwamba dhana hii itumike ikiwa na kivumishi kinachoeleza uhusika wa namna gani unaokusudiwa kila mara. Unaweza kuwa uhusika wa kimuundo au ushiriki wa kisemantiki. Aina hizi mbili za uhusika zina maungano katika matumizi. Mwangaza juu ya jambo hili unapatikana katika mkabala wa kiisimu wa Kaida na Vigezo na mwendelezo wake katika Uminimalisti. Kwa kutumia kauli ya kutendea, nitaelezea umuhimu wa kutofautisha maana hizo mbili.

Hoja hii inaletwa katika sehemu 4 zifuatazo. Katika Sehemu ya 2, nitaelezea Nadharia ya Uhusika kama ilivyo katika Mkabala wa Kaida na Vigezo. Nadharia

hiyo itaweka msingi wa mjadala juu ya uhusika wa yambwa za kutendea. Sehemu ya 3 inafafanua muundo wa kutendea. Sehemu ya 4 itajikita zaidi katika kuchanganua uhusika wa ala katika kauli hiyo, na Sehemu ya 5 itakuwa na hitimisho.

Nadharia ya Uhusika

Waandishi wengi wanaelezea kwamba dhana ya uhusika inavyotumika imepokelewa kutoka katika kazi ya Fillmore (1968) (tazama, kwa mfano, TUKI, 1990; Massamba, Kihore and Hokororo, 1999). Wazo kuu la Fillmore ni kuonesha kwamba kuna uhusiano wa kisemantiki baina ya kitenzi au hali na wahusika wa tukio linalowakilishwa na kitenzi. Uhusiano huo anauita uhusika, na alitoa hoja kwamba uhusika huo uko hata katika Kiingereza, lugha ambayo viwakilishi vichache vinatoa ishara ya kuwapo kwa mfumo wa uhusika. Uhusika ni uhusiano wa ndani zaidi katika vishazi. Kwa jumla, wataalamu wengine wengi wanautambua uhusika wa namna mbili, yaani uhusika wa kimuundo na uhusika wa kisemantiki. Kwa mfano, Jespersen (1924) alitofautisha baina ya *grammatical case* na *concrete case*.

Wasomi wa Nadharia Zalishi-geuzi waliendeleza wazo la Fillmore kwa kulinoa zaidi kutofautisha aina mbili za uhusika: (a) uhusika wa kimofolojia, na (b) uhusika dhahania. Wazo hili limependekezwa na wasomi, wakiwemo Chomsky (1981, 1995), Chomsky & Lasnik (1993), na Adger (2003). Wazo kuu la uhusika wa kimofolojia ni kwamba kuna lugha, kama vile lugha nasaba ya Kihindi-Kizungu na lugha za asili za Australia, zina viambishi vinavyoashiria nafasi ya nomino katika tungo. Mfano kutoka Kilatini unaonesha sifa hiyo ya kimofolojia. Neno *insula* ‘kisiwa’, linaambishwa hivi:

(4) kiolezofaridi cha *insula* ‘kisiwa’

	Umoja	Uwingi
U. kiima	<i>insul-a</i>	<i>insul-ae</i>
U. yambwa	<i>insul-am</i>	<i>insul-ās</i>
U. milikishi	<i>insul-ae</i>	<i>insul-ārum</i>
U. tendea	<i>insul-ae</i>	<i>insul-īs</i>
U. jumui	<i>insul-ā</i>	<i>insul-īs</i>

Mzizi wa maneno haya ni *insul* ‘kisiwa.’ Kiambishi tamati *-a* kinatambulisha neno la umoja linapokuwa katika nafasi ya kiima, ilhali kiambishi *-am* ni kiambishi tamati nomino hiyo inapokuwa katika nafasi ya yambwa. Nomino yoyote, iwe na dhima ya kutenda au kutendwa, inapokuwa katika nafasi ya kiima, inabeba kiambishi tamati cha uhusika kiima. Uhusika kiima si dhana ya kisemantiki, bali ni dhana ya kimuundo. Nomino inapata alama ya uhusika huo kwa sababu ya kuwa katika nafasi ya kiima. Orodha ya uhusika hapo juu (1) na (2), na katika lugha

mbalimbali, inaonesha dhahiri kuwa kuna baadhi ya uhusika hubeba nguvu ya kisemantiki na si uamilifu tu. Kwa mfano, uhusika tendea una maana ya nomino ambayo kwayo kuna kitenzi kimeelekezwa. Katika lugha hiyo, kila nomino iliyo katika tungo, lazima iwe na kiambishi cha kuonesha nafasi yake ya kimuundo na maana. Huu ndiyo uhusika wa kimofolojia.

Walakini si lugha zote zenye kuonesha uamilifu kwa kutumia viambishi kwenye nomino. Lugha nyingine hutumia upatanisho wa kisarufi au mfuatano wa maneno kuonesha uamilifu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Kaida na Vigezo, lugha zote zina mfumo wa uhusika unaotaka kila nomino iwe imekaguliwa na kuthibitishwa katika nafasi yake. Sifa hiyo inaweza ikaonekana hata haina mofolojia ya kuonesha uhusika. Katika Kiingereza, kwa mfano, kuna tungo kama hizi:

- (5) a. She designed the engine.
'Alisanifu injini.'
- b. The engine was designed by her.
'Injini ilisanifiwa naye.'
- c. John employed her.
'John alimwajiri.'

Viwakilishi viwili tofauti vinaonekana mbadala wa mtu yuleyule ambaye ni mwanamke. Katika (5a), kiwakilishi *she* kinaashiria uamilifu wa kiima; lakini kiwakilishi *her* kinaashiria nafasi ya yambwa (5c) na yambwa ya kihusishi (5b). Kwa jumla, nomino katika Kiingereza hazina kiambishi cha kuonesha uamilifu. Mabadiliko haya ya viwakilishi yanadhahirisha uwepo wa uhusika dhahania. Kwa maneno mengine, uhusika hujidhihirisha kimofolojia katika baadhi ya lugha, lakini lugha zote zina mfumo wa uhusika.

Kama ilivyo katika Kiingereza, mofolojia ya uhusika katika Kiswahili haina mifano mingi. Mfano mmoja dhahiri ni wa viambishi vya uwakilishi vya nafsi ya pili (umoja na uwingi), na nafsi ya tatu umoja.

- (6) Nafsi ya pili umoja
- a. Unaandika.
- b. Anakuona.

- (7) Nafsi ya pili uwingi
- a. Mnaona.
- b. Anakuoneni/Anawaoneni

- (8) Nafsi ya tatu umoja
- a. Anaona
- b. Namwona

Katika mfano (6a), kiambishi *u-* kinawakilisha nafsi ya pili umoja, lakini nafsi hiyo hiyo inawakilishwa na *-ku-* katika (6b). Tofauti ni kwamba katika (6a), kiambishi cha nafsi ya pili umoja ni kiima, ilhali katika (6b) kiambishi cha nafsi ya pili umoja ni kiwakilishi cha yambwa. Vivyohivyo, tunaona tofauti ya nafsi ya pili uwingi kiima *m-* (7a), na nafsi ya pili uwingi yambwa *-ku-* (7b). Nafsi ya tatu umoja yambwa inaonekana *a-* (8a) na inapokuwa yambwa, inakuwa *m-* au *mw-* (8b). Mifano hii si ya mofolojia ya uhusika, bali ushahidi kwamba hata kama lugha haina mofolojia ya uhusika, athari za mifanyiko ihusuyo uhusika huonekana.

Ilibainika kwamba, katika nafasi ambazo nomino haiwezi kupata kiambishi cha uhusika, hakuna nomino inayoonekana hapo. Jambo hili lilionekana kuwa sambamba katika lugha ambazo hazina uhusika wa kimofolojia. Jambo hili linaelezwa katika kaida moja ya uhusika inayokusudia kuwakilisha wazo la ulazima wa uhusika. Inasema:

(9) Kaida ya uhusika

Kila kirai nomino chenye kuonekana katika kiambajengo, lazima kiwe na uhusika (Chomsky, 1981:49)

Sambamba na kaida hii, kuna nafasi ambazo zilitambuliwa kuwa hazina uhusika dhahania unaohitajika kuidhinisha kirai nomino. Kwa mfano, imegundulika kwamba uhusika wa kiima unategemea kuwapo kwa njeo katika kirai njeo (KNj). Muundo usio na njeo au mofimu inayohusu halinjeo hauwezi kuidhinisha kirai nomino (KN) katika nafasi ya kiima. Kitenzi kisichokikomo hutambuliwa kuwa hakina njeo yenye kuthibitisha nafasi ya yambwa.

- (10) a. Halima alitaka [kk kuondoka].
b. *Halima alitaka [Juma kuondoka].
c. Halima alitaka [Juma aondoke]

Kitenzi cha ondoka huchukua uhusika mmoja wa mtenda; lakini kirai cha mtenda lazima kiidhinishwe na njeo, halinjeo au hali, kama ilivyo katika (10c). Hali tegemezi imewezesha nomino *Juma* kutokea katika kishazi tegemezi, bali hakikuruhusiwa katika (10b). Sentensi (10a) inawezekana kwa sababu kuna kategoria kapa (kk) katika nafasi ya kiima. Kwa hivyo basi, katika kishazi cha mfano hapa, kitenzi huidhinisha uhusika wa yambwa na njeo huidhinisha uhusika wa kiima, kama inavyooneshwa katika kielelezo hiki.

Nomino kaka ina ushiriki wa mtenda na ipo katika nafasi ya uhusika ya kiima, nafasi ya kimuundo iliyoidhinishwa na njeo. Nomino kiazzi, kwa upande mwingine, ina tafsiri ya ushiriki wa mtendwa na ipo katika nafasi ya kimuundo ya yambwa. Uhusika wa kiima unategemea muundo wa sentensi. Sentensi mbili za (12) zina washiriki walewale wa θ . Sentensi (12a) mtenda ndiyo kiima, na katika (12b), mtendwa ndiyo kiima. Zote mbili zikiwa mwafaka na kaida ya ushiriki ambayo inasema:

(14) Kila nomino katika tungo, lazima iwe na ushiriki wa theta (Chomsky 1981:36).

Kwa muhtasari, uhusika ni dhana ya kimuundo, ambapo kila kirai nomino katika kishazi lazima kiwe katika nafasi ya uhusika. Uhusika unaweza kuoneshwa kimofolojia au waweza kuwa dhahania. Nafasi hizo za uhusika hujazwa na nomino ambazo zinateuliwa na kitenzi kama ushiriki katika tukio. Ushiriki huu ni wa kisemantiki. Kauli ya kutendea inateua ushiriki wa namna anuai, lakini hauna nafasi nyingi za uhusika. Jambo hili linajadiliwa katika sehemu mbili zifuatazo:

Ufafanuzi wa Tungo za Kutendea

Tungo za kutendea huundwa kwa kiambishi kinachonyambulisha kitenzi na kukifanya cha kutendea na kikiwa na yambwa mpya. Mfano (15a) unaonesha tungo ya kutenda na (15b) unaonesha tungo ya kutendea.

- (15) a. Kaka alipika viazi.
b. Kaka aliwapikia watoto viazi.

Jozi hii ya mlingano finyu inadhahirisha sifa bainifu za tungo ya kutendea. Sifa ya kwanza ni kwamba tungo hii imeundwa na kitenzi ambacho kimeambikwa kiambishi cha unyambulishaji cha utendea {-i-}. Kwa hivyo, kitenzi cha *pika* kimenyambuliwa na kuwa *pikia*. Sifa ya pili inayotokana na unyambulishaji huo ni ongezeko la yambwa ya kitenzi hicho. Kitenzi *pika* kina washiriki wawili, mtenda *kaka* na mtendwa *viazi*. Nitaiita yambwa hii yambwa ya kitenzi kwa sababu uwepo wake unatokana na uteuzi unaofanywa na mzizi wa kitenzi. Kitenzi kilichonyambulishwa, *pikia*, kina washiriki watatu, mtenda *kaka*, kiathirika *viazi*, na mnufaika *watoto*. Mnufaika ni yambwa mpya inayotokana na unyambulishaji. Nitaiita yambwa hii yambwa ya kutendea. Mabadiliko ya uhusika huleta mabadiliko ya uamilifu. Katika sentensi ambayo kitenzi chake hakikunyambulishwa, *viazi* ndiyo yambwa pekee, lakini katika (15b), mhusika mpya *watoto* ndiyo sasa yambwa ambayo hata inaonekana katika upatanisho wa kisarufi wa yambwa katika kitenzi. Ushiriki wa yambwa tendea ni wa anuai na kuufanya muundo huu kuwa uwanja wa data jarabati kuhusu uhusika.

Kama ilivyokwishasemwa, kauli ya kutendea inatokana na kunyambua kitenzi kwa kutumia kiambishi cha kutendea. Kiambishi cha kutendea kina alomofu nne. Alomofu mbili *-i* na *-e* zinaonekana katika mifano katika Na. (2).

(16)	lip-a	lip-i-a
	let-a	let-e-a
	kat-a	kat-i-a
	som-a	som-e-a
	vun-a	vun-i-a

Alomofu hizo zinatokana na tangamano la irabu. Mashina yenye /a/, /i/ au /u/ yatachukua alomofu *-i*, na mashina yenye /e/ au /o/ yatachukua kiambishi *-e*. Irabu ya kiambishi hufuatisha sifa ya mwinuko wa irabu ya shina. Kwa mfano, katika shina *soma*, irabu ya shina ni /o/. Kwa hivyo, kiambishi cha kutendea kitakuwa katika ngazi hiyo ya kati. Endapo irabu ya shina ni /a/, basi tangamano la irabu haliwezi kudhihirika. Kwa sababu hiyo, tunapata *kata - katia*. Tangamano hilo la irabu linaweza kuwasilishwa kama ilivyo katika (17).

(17) Tangamano la irabu ya kutendea

	Mbele	Nyuma		Kiambishi
Juu	i	u	→	-i
	e	o	→	-e
Chini	a		→	-i

Zipo pia alomofu nyingine mbili ambazo, kwa kiasi kikubwa, zinafuata tangamano la irabu. Alomofu hizo ni *il* na *-el*. Katika mifano ifuatayo, alomofu hizo zinatokea kabla ya kiambishi cha kutendesha²⁰.

(18)	enda	end-el-ez-a
	tosha	tosh-el-ez-a
	pita	pit-il-iz-a

Wataalamu wengine hawazitambui alomofu *-il* na *-el*; badala yake, wanasema alomofu za kutendea ni *-li* na *-le* (Habwe na Karanja, 2004; Wesana-Chomi, 2013). Mifano hii inatilia shaka uchambuzi huo, kwani itatupasa kufanya *ende* kuwa mzizi na si *ende* kama kitenzi *endeleza* hapo juu.

²⁰ Ni muhimu kukumbuka kwamba si kila kitenzi chenye kiambishi *-ez* au kiambishi cha kutendesha kinakuwa na maana ya kutendesha hasa. Polisemia inafanya viambishi mbalimbali viwe na maana zenye tofauti kidogo na maana kifani. Sifa hii ya polisemia ya vipashio ni ya kawaida katika lugha (Taylor, 2003).

Sababu nyingine ya kuzitambua *-il* na *-el* kama alomofu ni vile ambavyo /l/ inaonekana tena na tena kuhusika na viambishi vingine vya unyambulisho, hususan kutendeka na kutendesha.

(19)	tambua	tambulika
	kaa	kalika
	fagia	fagilika
	zoa	zoleka
	zuia	zuilika
	zoea	zoeleka

(20)	tambua	tambulisha
	kaa	kalisha
	jua	julisha
	zaa	zalisha
	noa	nolesha

Kwa hakika, /l/ ni sehemu ya shina nayo huonekana tu pale ambapo kuna kiambishi kingine cha kunyambulisha. Kwa hivyo, kiambishi cha kutendeka ni *-ik* na *-ek*; na kile cha kutendesha ni *-ish*, *-esh*, *-iz*, na *-ez*. Ninaafikiana na wanaisimu wengine kama Schadeberg (1973), Khamis (2008), na Kihore na wenzake (2009). Pia, ni mwafaka na wazo la wanaisimu waliothibitisha kwamba alomofu ya awali ilikuwa /-il/. Fonimu /l/ imedondoshwa katika mazingira mengi (Nurse & Hinnebusch, 1993:370). Mofimu kutendeka inaaminika ilikuwa **-id* katika Mame Bantu (Meeussen, 1967).

Badiliko linalotokana na kiambishi cha kutendeka ni kuongeza yambwa mpya, kama ilivyosemwa hapo awali. Jambo hili linasababisha mabadiliko ya uamilifu wa virai nomino katika sentensi. Mabadiliko hayo yanaweza kuoneshwa kwa kutumia mifano ya vitenzi viwili vinavyonyambulishwa. Vitenzi hivyo ni *kimbia* na *pika* kama ilivyo katika tungo zifuatazo.

- (21) a. Kaka alikimbia.
b. Kaka aliwakimbilia watoto.

- (22) a. Kaka alipika viazi.
b. Kaka aliwapikia watoto viazi.

Kitenzi *kimbia* (21) kinaelezea mtenda *kaka* na alichokifanya *alikimbia*. Kitenzi hicho kinaponyambulishwa (21b) na kuwa *kimbilia*, kinakuwa na lengo la tukio la kukimbia. Katika makala hii, tutawaita mtenda na mtendwa kuwa ni washiriki. Nafasi za uamilifu wa kisintaksia ni kama kiima na yambwa. *Kaka* ni kiima na *watoto* ni yambwa. Katika mfano (22), kitenzi chetu ni *pika* nacho kina washiriki

wawili, *kaka* na *chakula*. Kikinyambulishwa na kuwa *pikia*, kinakuwa na washiriki watatu, *kaka*, *chakula* na *watoto*. Mabadiliko hayo yanaoneshwa katika vielelezo kwa kutumia mirabafito. Kwa kila kitenzi, taarifa kuhusu mambo matatu zinaoneshwa: kwanza uamilifu (kiima, yambwa), pili ni ushiriki (mtenda, mtendwa), na juu kabisa ni mfano wa nomino zilizopo katika mifano yetu hapo juu (21) na (22).

(23) Mirabafito ya uhusika

Kimbia	Kitenzi	Kaka		Mshiriki 1	
		Mtenda			
		Kiima			
kimbilia	kitenzi	Kaka	Watoto	Washiriki 2	
		mtenda	Lengo		
		Kiima	Yambwa		
Pika	kitenzi	Kaka	Chakula	Washiriki 2	
		mtenda	Kitendwa		
		Kiima	Yambwa		
pikia	Kitenzi	Kaka	Chakula	Washiriki 3	
		mtenda	Kitendwa		watoto
		Kiima	Yambwa		kitendewa

Kitenzi chochote kinaponyambulishwa na kiambishi cha kutendea kinapata mshiriki mmoja mpya. Kila kitenzi kina mahitaji ya kuunganishwa na idadi fulani ya wahusika. Kwa hivyo, kila kitenzi kina muundo wa ushiriki. Muundo wa ushiriki wa *pika*, kwa mfano, ni washiriki wawili, wakati muundo wa ushiriki wa *pikia* ni washiriki watatu. Kitenzi *pika* kinaungana na mtenda *kaka* na mtendwa *chakula*. Kinaponyambulishwa na kuwa *pikia*, kinaungana na *kaka*, *chakula* na *mtoto*. Katika sentensi (22a), yambwa *chakula* inadhihirika kwa upatanisho wa kisarufi kwa kiambishi *ki-*. Kiambishi hiki kinabadilishwa na kuwa *wa-* kuwakilisha mtendewa katika (22b).

Uhusika wa yambwa mpya unaweza kupata tafsiri mbalimbali tofauti. Jambo hili limetajwa na wachunguzi wengi (tazama, kwa mfano, Bresnan & Moshi, 1990; Ngonyani, 1996; Mabugu, 2001; Sibanda, 2016; Pacchiarotti, 2017). Mifano ifuatayo inayotoka kwa Ngonyani (1996) inadhihirisha jambo hili:

- (24)
- a. Mama aliwapikia watoto chakula. (tendea)
 - b. Msichana aliwasukumia kuku jongoo. (lengo)
 - c. Nyani aliwamalizia wawindaji maji. (mwathirika)
 - d. Mawe walivunjia chungu. (ala)
 - e. Wawindaji waliwindia pesa. (sababu)

- f. Wawindaji walichunia nyama manyasini. (mahali)
- g. Mpishi aliungia nyama pilipili (malighafi)

Mifano hii inaonesha kwamba kauli ya kutendea inawezesha aina tofauti za ushiriki wa yambwa mpya. Ushiriki pekee ambao hauonekani kuletwa na kauli ya kutendea ni wa mtenda.

Muundo wa tungo za kauli ya kutendea umezua mijadala mingi, hasa kwa mtazamo wa kinadharia unaozingatia jambo moja la msingi. Jambo hilo ni kwamba, ijapokuwa lugha zinatofautiana sana, tofauti hizo si za holela, bali zinafuata kaida au kanuni fulani na vigezo. Miongoni mwa machapisho yaliyoleta mwanga mkubwa kuhusu kutendea ni makala ya Bresnan & Moshi (1990). Mchango mkuu wa makala hiyo ni kuainisha lugha za Kibantu katika makundi mawili kwa mujibu wa kauli ya kutendea. Katika kundi moja, lugha kama Kichaga, uhusiano wa yambwa mbili ni wa upacha. Katika lugha hizo, yambwa ya kitenzi na yambwa ya kutendea zote huweza kuwa kiima cha kauli ya kutendwa, hufanya upatanisho wa kisarufi wa yambwa, pia huweza kuwa karibu na kitenzi. Aidha, katika kundi la pili, lugha kama Kichewa, yambwa mbili zina uhusiano usopacha. Yambwa ya kutendea ndiyo inayoweza kuwa kiima cha kauli ya kutendwa ambacho hufanya upatanisho wa kisarufi na kitenzi, na huwa karibu zaidi na kitenzi. Sifa hizi zinajidhihirisha katika maumbo kadhaa ya kimuundo.

Marantz (1993) aligundua kwamba yambwa za muundo usopacha wa tungo za kauli ya kutendea zinaonesha sifa ambazo ni sawa na zile za tungo za yambwa mbili katika lugha kama Kiingereza, lugha ambayo haina mofimu ya kutendea. Kwa kutumia ufungami, Marantz anaonesha kwamba, katika lugha ya Kiswahili, yambwa tendea inaweza kufungama yambwa ya kitenzi, lakini yambwa ya kitenzi haiwezi kufungama yambwa tendea.


(25) Ufungami wa yambwa mbili

- a. Ni-li-m-som-e-a [kila mw-andishi]_i kitabu chake_i
- b. *Ni-li-m-som-e-a mw-andishi wake_i [kila kitabu]_i

(Marantz, 1993:116 -117)

Katika sentensi (25a), *kila mwandishi* ni yambwa tendea na *kitabu chake* ni yambwa ya mzizi wa kitenzi. Sentensi hiyo inaonesha kwamba inawezekana kwa yambwa mpya kufungama yambwa ya mzizi, kama ilivyooneshwa kwa alama za *i* ndogo. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uunganifu, kufungama kunawezekana tu pale ambapo kirai kinachokifungama kingine kinapokuwa juu zaidi katika muundo msonge. Kushindikana *kila kitabu* kufungama kila mwandishi katika (25b) ni ushahidi

kwamba, yambwa ya kitenzi haiko katika nafasi ya juu zaidi ya kitendea. Ndiyo kusema yambwa tendea huzalishwa katika kifundo juu zaidi ya kifundo kinachozalisha yambwa ya kitenzi. Marantz anapendekeza kwamba kiambishi cha kutendea kina hadhi kama ya kitenzi. Hii inatokana na sababu kuwa nacho kinachagua kirai tenzi na yambwa tendea, kama inavyooneshwa hapa:



(Marantz, 1993:119)

Kwa uchambuzi huu, kitenzi husogezwa na kuunganishwa na kichwa kipya cha kutendea. Utambuzi wa kiambishi hiki kuwa kichwa cha kirai unakubaliana na uchambuzi wa Baker (1988) na Kayne (1994). Muundo huu usopacha uliungwa mkono na Ngonyani (1996) aliyetumia kiunzi cha viambajengo vya udondoshaji. Katika tasnifu yake, anabainisha kwamba muundo huu ni uhusika wowote. Majaribio ya Ngonyani na Githinji (2006) yalithibitisha kwamba muundo usopacha ni wa msingi hata kwa lugha kama Kikuyu ambayo ina yambwa za utendea zilizopacha.

Uchambuzi huu wa muundo usopacha umekubalika kwa wengi wanaochunguza tungo za kauli ya kutendea kwa mkabala wa Kaida na Vigezo. Hata hivyo, unaibua maswali mengi mengine. Mojawapo ya maswali hayo ni chanzo cha tofauti za kisintaksia za yambwa mbalimbali. Yambwa tendea ya ala ina tabia za kutatanisha, kama inavyojadiliwa katika sehemu ifuatayo.

Uhusika na Ushiriki wa Ala

Uhusika wa ala si wa aina moja. Kwa kutumia mifano ifuatayo, tafsiri mbalimbali za uhusika wa ala unadhihirika.

- (27)
- a. kijiko alilia wali.
 - b. kisu alikatia muwa.
 - c. wali waliungia tui la nazi.

Katika sentensi (27a), mtu alikula, na zana au ala hii ilimsaidia katika kula. Sentensi (27b), kwa upande mwingine, ina maana ya mtu alikifanya kisu kikate. Hapa kuna usababishi. Na katika (27c), yambwa tendea si kifaa hasa, bali ni kama kile Habwe na Karanja (2004) walichokiita malighafi.

Kutokana na tofauti zinazoonekana katika mifano 27a-c, Ngonyani (1996) anapendekeza kwamba muundo wa kauli ya kutendea unaohusu ala una vishazi viwili, kimoja kikiwa tegemezi. Anaonekana kuamini kwamba tofauti za aina hizo mbili za ala ni za kimuundo, na anapendekeza uchambuzi wa tungo zenye ala hizo tofauti kuwa hivi:

- (28) a. Mtoto [kwa kisu SABABISHA [kata muwa]]
b. Mtoto [kijiko TUMIA [kunywa supu]]
(Ngonyani, 1996:173)

Katika mfano wa kwanza, mtoto anasababisha kisu kikate muwa. Ni kisu hasa ndicho kinachokata. Muundo huu unaonesha kishazi tegemezi ambacho kiima chake ni *kisu*. Kisu ni kama wakala baina ya *mtoto* na yambwa *muwa*. Katika mfano wa pili, mtoto anakunywa supu. Kiima cha kishazi tegemezi hiki ni *mtoto*.

Zaidi ya kutoa pendekezo hili, hakuna hoja na ushahidi zaidi wa chanzo cha tofauti tuzionazo. Kinachooneshwa katika uchambuzi huu ni tafsiri tu na wala hakuna ushahidi wa kisintaksia wa kuonesha vishazi tegemezi. Tunatarajia kwamba, ufafanuzi wake ungepelekea kuonesha kwamba tofauti zinazoonekana katika fasili ya tungo inatokana na miundo tofauti inayotokana na kitenzi. Hata hivyo, hata kwa kutumia kitenzi *pikia* tunaona uko uwezekano wa kupata uhusika wa aina mbalimbali wa yambwa tendea. Kwa mfano:

- (29) a. Kaka aliwapikia watoto wali,
b. Kaka alipikia wali tui la nazi, na
c. Kaka alipikia wali jiko la gesi.

Tofauti hizi za maana za kutendea hazitokani na muundo. Zinatokana na maana za msingi za kitenzi *pika* pamoja na maana msingi za viima vyenyewe. *Pikia watoto wali*, kwa mfano, haiwezi kupelekea kutafsiri kwamba *watoto* walikuwa kiungo kama ambavyo *tui la nazi* lilikuwa. Halikadhalika, *jiko la gesi* haliwezi kuchukuliwa kwamba ndiyo mfaidika wa kitendo cha kupika. Kwa hivyo basi, tofauti za maana zisitafutwe katika miundo, bali katika maana za washiriki wenyewe na kitenzi.

Katika hali halisi, hoja hii inaimarisha hoja ya Sibanda (2016) anayesema kwamba sehemu kubwa ya maana ya ushiriki au theta ya yambwa tendea inatokana na maana ya kitenzi. Iwapo kitenzi kinahusu usogeaji wa kitu, kwa mfano, basi kiima tendewa kitakuwa na tafsiri ya lengo au mahali au ala. Tafsiri ya lengo haitokei kwa vitenzi ambavyo havihusu kusogea kwa kitu. Hebu tuangalie mifano zaidi.

- (30) a. Kaka alipikia chakula uwanjani.
b. Kaka alitupikia chakula.

- (31) a. Kaka alimfagilia mzee uwanja.
b. Kaka alimfagilia mzee maganda.

- (32) a. Fundi aliwakatia watu umeme.
b. Fundi aliwakatia watu mihogo.

Tuliona katika sentensi za (30) maana tatu tofauti za ala zilipatikana kwa kiima tendewa cha *pikia*. Katika sentensi (30a), kwa upande mwingine, *pikia* inachagua yambwa ya mahali, na yambwa ya mtendewa katika (30b). Yambwa za *fagilia* nazo zinaleta maana mbili tofauti. Katika (31a), yambwa cha kitenzi ni *uwanja*. Yambwa hiyo inapobadilishwa na kuwa *maganda*, tafsiri nyingine ya ushiriki hunyemelea. Inawezekana kabisa kutafisiri kwamba mzee alikuwa lengo la kule zilikopeleka takataka. Kitenzi *katia* kimetumika katika (32). Katika sentensi zote mbili, kiima kipya ni *watu*. Hata hivyo, maana mbili tofauti zinapatikana. Katika (32a), *katia umeme* inaeleweka kwamba watu ni waathirika wa kitendo hasi. Uhasi huo si dhahiri katika (32b), ambapo tafsiri ya moja kwa moja ni kwamba watu walipokea vipande vya mihogo.

Kwa kifupi, ushahidi tulioutoa hapa unaonesha kwamba tofauti za maana ya yambwa zenye kutafsiriwa kama ala hazizalishwi na muundo wa vipashio mbalimbali vinapounganishwa; bali, zinatokana na maana ya msingi ya kitenzi na, hata nomino au kiima chenyewe katika muktadha wake. Hizi ni tofauti za ushiriki na za kisemantiki.

Tofauti hizi haziwiani na tofauti za uhusika. Uhusika wa yambwa mpya hiyo unaonekana katika mfululizo wa yambwa katika tungo hizo. Nitajaribu kuweka yambwa zote mbili katika nafasi baada ya kitenzi.

- (33) a. ?Mtoto alilia kijiko wali.
b. ?Mtoto alikatia kisu muwa.
c. ?Kaka aliungia tui la nazi wali.

Kwa maoni yangu, sentensi hizi zina ukakasi kidogo. Ndiyo maana nimeweka alama ya kuuliza mwanzoni mwa kila sentensi. Inaonekana kwamba ushiriki wa yambwa tendea ukifasiriwa kuwa ni mnufaika kama (15b) hapo juu, yambwa tendea na yambwa ya kitenzi huweza kuonekana pamoja. Tena, yambwa tendea hukalia nafasi kabla ya yambwa ya kitenzi. Jambo hili haliwezekani iwapo yambwa tendea ni ala au malighafi kama inavyooneshwa (33). Inaonekana kuna nafasi ya uhusika mmoja tu baada ya kitenzi.

Kwa kuhitimisha, uhusika ala unahusu ushiriki wa namna zisizopungua tatu. Uhusika huo unaonekana kwa kutoruhusu yambwa mbili kuonekana pamoja baada ya kitenzi na; badala yake, kupendelea yambwa moja iwekwe mwanzoni. Tofauti baina ya uhusika wa kimuundo na ushiriki wa kisemantiki inaonekana.

Hitimisho

Makala hii imetalii dhana ya uhusika. Kwa kutumia mkabala wa Kaida na Vigezo, nimetofautisha uhusika kama dhana ya kimuundo na ushiriki kama dhana ya kisemantiki. Uhusika unaweza kuwa wa kimofolojia au dhahania. Kiswahili hakina uhusika wa kimofolojia ijapokuwa matokeo ya uhusika dhahania honekana katika miundo mbalimbali. Kwa kutumia kazi za watangulizi, makala imeonesha kuna tafsiri anuwai za yambwa za kutendea. Baada ya kutalii ushiriki mbalimbali unaotokana na tungo hizo, makala ilitumia uhusika wa ala ili kuwasilisha hoja tatu. Hoja ya kwanza ni kwamba, tafsiri ya uhusika wa yambwa inategemea sana mzizi wa kitenzi. Pili, mara kwa mara, tafsiri zinatokana na hulka ya yambwa au tunavyotarajia katika muktadha wa mazungumzo. Hoja ya tatu ni kutilia shaka uchambuzi unaoelekea kudai kwamba tofauti za tafsiri ya ala inatokana na miundo tofauti. Pamoja na yote, mjadala wa mchango wa vitenzi katika kuleta maana tofauti za yambwa mpya unahitaji kupanuliwa zaidi.

Marejeleo

- Adger, D. (2003). *Core Syntax: A Minimalist Approach*. Oxford: Oxford University Press.
- Baker, M. (1988). Theta theory and the syntax of applicatives in Chichewa. *Natural Language and Linguistic Theory*, 6, 353-389.
- Bresnan, J., & Moshi, L. (1990). Object asymmetries in comparative Bantu. *Linguistic Inquiry*, 21(2), 147-185.
- Chomsky, N. (1981). *Lectures on Government and Binding*. Dordrecht: Foris Publications.
- Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Program*. Cambridge, MA: MIT Press.
- Chomsky, N., & Lasnik, H. (1993). The theory of principles and parameters. Katika J. Jacobs, A. von Stechow, W. Sternefeld, & T. Vennemann, *Syntax: An International Handbook of Contemporary Research* (uk. 506-569). Berlin: Walter de Gruyter.

- Fillmore, C. J. (1968). The case for case. In E. Bach, & R. Harms (Wahr.), *Universals in Linguistic Theory*. New York: Holt, Rinehalt, & Winston.
- Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Jespersen, O. (1924). *The Philosophy of Grammar*. Chicago: Chicago University Press.
- Kayne, R. (1994). *The Antisymmetry of Syntax*. Cambridge, MA: MIT Press.
- Khamis, A. M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Kihore, Y., Massamba, D. P., & Msanjila, Y. P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mabugu, P. R. (2001). *Polysemy and the Applicative Verb Construction in Chishona*. Edinburgh: University of Edinburgh.
- Marantz, A. (1993). Implications of the asymmetries in double object constructions. Katika S. A. Mchombo (Mhr.), *Theoretical Aspects of Bantu Grammar* (uk. 113-150). Stanford: Center for the Study of Language and Information.
- Massamba, D. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Massamba, D. P., Kihore, J. M., & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Meeussen, A. E. (1967). Bantu grammatical reconstructions. *Africana Linguistica*, III, 79-121.
- Ngonyani, D. (1996). *The Morphosyntax of Applicatives*. Los Angeles: UCLA Doctoral Dissertation.
- Ngonyani, D., & Githinji, P. (2006). The antisymmetric nature of Bantu applicatives. *Lingua*, 116, 31-63.
- Nurse, D., & Hinnebusch, T. (1993). *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. Berkeley: University of California Press.
- Pacchiarotti, S. (2017). *Bantu Applicative Construction Types Involving *-id: Form, Functions and Diachrony*. Tasnifu ya Uzamivu, Eugene: University of Oregon.
- Schadeberg, T. (1973). *A Sketch of Swahili Morphology*. Dordrecht: Foris Publications.
- Sibanda, G. (2016). The Ndebele applicative construction. Katika D. L. Payne, S. Pacchiarotti, & M. Bosire (Wahr.), *Diversity in African Languages* (uk. 309-333). Berlin: Language Science Press.
- Taylor, J. R. (2003). *Linguistic Categorization* (3 ed.). New York, NY: Oxford University Press.
- TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.